

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA



27/4/2022

## TANGAZO

### TANGAZO LA ZABUNI YA USAFISHAJI WA CHOO CHA MICHUNGWANI NA SOKO LA MITUMBA

1. Halmashauri ya muheza inawatangazia makampuni kuwa inahitaji kupata wazabuni wenye uwezo wa kusafisha choo cha michungwani na soko la mitumba kwa niaba ya Halmashauri kwa mujibu wa sheria ndogondogo za Halmashauri kama ilivyoainishwa hapo chini:-

ZABUNI NAMBA	JINA LA ZABUNI
LGA/132/2021/2022/NC/39	UWAKALA WA USAFISHAJI WA VYOO SOKO LA MITUMBA NA SOKO LA MICHUNGWANI.

### 3. Masharti kwa Waombaji:-

Mwombaji awe na uwezo wa kusafisha kusafisha choo cha michungwani na choo cha soko la mitumba

- i. Mfumo wa kielektroniki unaotumika na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ni Local Government Revenue Collection Information System – LGRCIS kwa ajili ya kukusanya ada ya tozo ya usafishaji choo.
- ii. Tozo ya ada itakayokusanywa itaingizwa katika Akaunti ya Halmashauri na wakala atalipwa . Muda wa malipo kwa wakala ni ndani ya siku saba [7] ya mwezi unaofuata baada ya wakala kuleta hati ya madai husika.(ambatanisha barua ya kukubali)
- iii. Wakala aonyeshe kiasi cha tozo atakachokusanya kwa mwezi.
- iv. Wakala aonyeshe asilimia itakayolipwa baina yake na Halmashauri pamoja na mchanganuo wa mapato,matumizi na faida.Na ikumbukwe kuwa kuweka kiwango kidogo cha asilimia ya malipo siyo kigezo pekee cha kupata zabuni mchanganuo wa mapato na matumizi ndio utakaotoa picha ya uhalishia wa kiwango cha gharama.
- v. Muombaji asiwe anadaiwa na Halmashauri
- vi. Muombaji awe na Leseni hai ya Biashara
- vii. Muombaji awe na usajili wa kuandikishwa kwa Kampuni/kikundi na kama ni kikundi kiambatanishe barua ya mtendaji wa kata na katiba ya kikundi.
- viii. Muombaji lazima atoe mchanganuo wa namna atakavyofanya usafi wa vyoo.
- ix. Muombaji awe na "Taxpayer Identification Number(TIN)"
- x. Muombaji aonyeshe uthibitisho wa kulipa kodi(TAX CLEARANCE)

- xi. Asilimia 20% itatozwa kwa wakala atakaye chelewesha marejesho yake ndani ya siku 5 kulingana na tarehe ya marejesho ya mkataba.
- xii. Muombaji aambatanishe uhalali wa kisheria (**Power of attorney**) wa mtu atayehusika na zabuni hii.
- xiii. Muombaji hatakiwi kuwa mtumishi au Kiongozi wa Halmashauri ya wilaya muheza.
- xiv. Uzoefu wa wataalamu au wafanyakazi atakao watumia katika kufanya kazi ya kukusanya ushuru kupitia wasifu wa kila mhusika (CV).
- xv. Wakala atakayeshinda zabuni hii atawajibika kuweka Dhamana ya utendaji kazi (performance bond financial) fedha taslimu, Wakala atakayeshinda zabuni hii atawajibika kuweka Dhamana ya utendaji kazi ya fedha taslimu za miezi mitatu anazotarajia kukusanya kwa mujibu wa memorandam
- xvi. Wakala atawajibika kuhakikisha vyoo vinakuwa safi muda wote wa utekelezaji wa mkataba.
- xvii. Kila mwombaji anatakiwa kufanya utafiti kwenye eneo la kusafisha vyoo na kuonyesha kiasi cha mapato atakachokusanya kwa kila mwezi
- xviii. Mwombaji awe na uzoefu katika ukusanyaji wa mapato usiopungua mwaka mmoja (ambatanisha barua za uteuziwa kazi hizo ,mkataba)
- xix. Mwombaji aonyeshe ilipo ofisi zake(pysical location)

#### **JINSI YA KURUDISHA ZABUNI**

Zabuni zitatumwa kwenye mfumo wa Taneps